PRAYER 316

# Je, Ni Jinsi Gani Napaswa Kuomba?

**Je, ni jinsi gani napaswa kuzungumza na Mungu?** Kuomba ni kuzungumza na Mungu. Biblia ni Mungu akizungumza nasi. Jifunze kile ambacho Biblia inatufundisha kuhusu maombi. *"Siku moja, Yesu alikuwa mahali fulani akiomba. Alipomaliza kuomba, mmoja wa wanafunzi wake akamwambia, 'Bwana, tufundishe kuomba,'"* Luka 11:1. Omba sala hiyo hiyo. Mafundisho ya Biblia kuhusu maombi yanajumuisha sifa, shukrani, ungamo, na kutaja matamanio yako. Sifa humuinua, humheshimu na kumtukuza Mungu, Zaburi 34:1-3. *"Nitamtukuza Bwana nyakati zote,"* Waebrania 13:15. Shukrani ni kwa sababu ya kile ambacho amefanya. *"Ni vyema kumshukuru Bwana,"* Zaburi 92:1. Ungamo ni kwa sababu ya dhambi yetu. *"Tukiziungama dhambi zetu, yeye ni mwaminifu na wa haki, atatusamehe dhambi zetu na kutusafisha kutokana na udhalimu wote,"* 1 Yohana 1:9. Taja matamanio yako kwa Mungu kwa sababu amekualika kufanya hivyo. *"Kwa kuomba na kusihi pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu,"* Wafilipi 4:6. Kumwomba Mungu akidhi mahitaji yako ya kimwili na kiroho ni jambo linalojumuishwa katika Sala ya Bwana iliyo katika Mathayo 6:9-13. Maombi ni fursa yako ya kipekee ya kuzungumza na Mungu aishiye. *"Macho ya Bwana huwaelekea wenye haki, na masikio yake yako makini kusikiliza kilio chao,"* Zaburi 34:15. *"Kwa hiyo kila mtu mcha Mungu akuombe,"* Zaburi 32:6.

**Je, napaswa kuomba wapi?** Ni vizuri kuomba katika majengo ya kidini na katika mikutano. Hata hivyo, Yesu alisema, *"Mungu ni Roho, na wote wanaomwabudu imewapasa kumwabudu katika roho na kweli",* Yohana 4:24. Maombi yenye ufanisi hayategemei mahali ulipo kimwili. Yesu alisema, *"Nanyi mnaposali, msiwe kama wanafiki, maana wao hupenda kusali wakiwa wamesimama katika masinagogi na kando ya barabara ili waonekane na watu. Amin nawaambia, wao wamekwisha kupokea thawabu yao. Lakini wewe unaposali, ingia chumbani mwako, funga mlango na umwombe Baba yako aliye sirini. Naye Baba yako aonaye sirini atakupa thawabu yako,"* Mathayo 6:5-6. Maombi yenye ufanisi hayategemei mahali unapoomba. Yanategemea hali ya moyo wako. Omba hadharani. Omba faraghani.

**Je, napaswa kuomba nikiwa nimepiga magoti?** Yesu na Danieli walipiga magoti, Luka 22:41, Matendo 20:36, na Danieli 6:10. Omba ukiwa umepiga magoti. Hata hivyo, watu wengine katika Biblia walisimama, walitazama anga, walinyoosha mikono yao kando au juu, waliinama chini, na walisimama mbele ya ukuta. Mkao wa mwili ni muhimu katika maombi ikiwa tu unaonyesha hali ya moyo wako.

**Je, ni jinsi gani napaswa kuomba?** *Jinsi* ya kuomba ina umuhimu sawa, au ni muhimu zaidi kuliko *kile* unachoombea. Maombi ya kibiblia ni kummiminia Mungu yaliyo moyoni mwako kwa uwazi na kwa ukweli. Hakuna michanganyiko maalum ya maneno, virai, au sentensi unayopaswa kutumia katika maombi, au unayoweza kusema, ambayo itamlazimisha Mungu kukupa kile unachomwomba. Maagizo ya Biblia na mifano yake inajumuisha kuomba:

Kwa moyo wa shukrani, 1 Wathesalonike 5:18.

Ukiwa mkweli, si kukariri tu sala fulani uliojifunza, Isaya 29:13.

Bila kujirudiarudia kwa njia isiyo na maana, Mathayo 6:7.

Kwa uwazi, moja kwa moja, na ukiwa mkweli Isaya 37:14-17.

Kwa kujitoa kwa dhati na kwa uvumulivu, Wakolosai 4:2, Luka 11:5-10, 18:1-8.

Bila kukoma, 1 Wathesalonike 5:17.

Kwa bidii kuu, Warumi 15:30.

Kwa umoja na Waumini wengine, Mathayo 18:19-20, 1 Timotheo 2:8.

Kwa imani kuu, Yakobo 1:6-7, Waebrania 11:6.

Kulingana na mapenzi ya Mungu, Yohana 15:7, 1 Yohana 5:14-15.

Kwa jina la Yesu, kulingana na mapenzi yake kama mwakilishi wake, Yohana 14:13, 15:16.

**Je, napaswa kuombea nini** Katika Sala ya Bwana, Yesu aliwafunza wanafunzi wake kuomba kila siku kwa ajili ya mahitaji yao ya kimwili na ya kiroho. Katika sala yake iliyo katika Yohana 17, Yesu alijiombea yeye mwenyewe, aliwaombea wanafunzi wake, na aliombea ulimwengu. Yesu aliahidi kwamba maombi ya uaminifu, yanayoendana na mapenzi yake, yalioelekezwa kwa Baba, katika jina lake, yatajibiwa, Yohana 15:7, 16, 16:23, 1 Yohana 5:14-15. Maagizo mengine ya kibiblia na mifano ya kile unachopaswa kuombea ni pamoja na:

Hekima, Yakobo 1:5, 2 Mambo ya Nyakati 1:7-12.

Ustawi wa kiroho, Wakolosai 1:9-12.

Wale wanaokutendea vibaya, Luka 6:28.

Uponyaji, unawezekana, Yakobo 5:14-15, lakini si kwa kila mtu, 2 Wakorintho 12:7-9.

Kuombeana sisi kwa sisi Waefeso 6:18, Yakobo 5:16.

Serikali yako, 1 Timotheo 2:1-2.

Chakula chako, Mathayo 6:11, Marko 6:41, 8:6-7.

Wale wanaomhitaji Kristo, Warumi 10:1.

Wafanyakazi wa kutangaza Injili, Mathayo 9:37-38.

Milango iliyofunguka kwa ajili ya Injili, Wakolosai 4:3-4.

**Mungu husikia na kujibu maombi yako.** Tosheleza masharti ya Mungu kwa ajili ya maombi na atakujibu. Jibu la Mungu linaweza kuwa *ndio, ndio iliyocheleweshwa,* au *la.* Anaweza kukupa zaidi ya kile unachoomba au kufikiria, Waefeso 3:20. Ndio ya Mungu iliyocheleweshwa huenda ni kwa sababu ya kukuandaa au kuwaandaa wengine kwa ajili ya jibu lake. Au jibu lake linaweza kuwa *la isiyobadilika.* Omba ukiwa na imani kwake na kuamini kabisa majibu yake.

Nia yako ni muhimu. *"Mnapoomba hampati kwa sababu mnaomba kwa nia mbaya, ili mpate kuvitumia hivyo mtakavyopata kwa tamaa zenu,"* Yakobo 4:3.

Mume, mtendee mke wako wema. Biblia inafundisha kwamba mume anapaswa kumpenda mke wake kama Kristo anavyolipenda kanisa, akimthamini, kuzingatia hisia zake, na kumheshimu kama mrithi mwenzake wa neema ya uzima, *"Ili kusiwepo na chochote cha kuzuia maombi yenu,"* 1 Petro 3:7.

Wasamehe wengine. Kutosamehe kunazuia maombi yako. Msamaha wako kwa wengine unaonyesha msamaha unaopaswa kutarajia kutoka kwa Mungu, Marko 11:25, Mathayo 5:23-24, 6:12-15.

Kuwa mwenye haki. Kuwa safi mbele za Mungu ili maombi yako yapate matokeo makubwa. *"Maombi ya wanyofu humfurahisha Mungu,"* Mithali 15:8. Hata hivyo, ikiwa mtu ataasi sheria ya Mungu, *"Hata maombi yake ni chukizo,"* Mithali 28:9. Mungu hukulinda, hukuandaa, na kukukamilisha. Kukataa kwa Mungu na kuchelewa kwake kukupa kile unachoomba kunaweza kuwa ni kwa wema wako.

Mungu hukulinda wakati hujui kwamba kile unachoomba kinaweza kukudhuru. Mungu anakujua vyema zaidi kuliko jinsi unavyojijua. Wakati mwingine Mungu husema hapana kwa sababu anajua maisha yako ya baadaye na anajua kile kilicho bora zaidi kwako. Wakati mwingine kucheleweshwa ni kwa sababu ya kukupa muda wa kujiandaa kwa jibu lake. Wakati mwingine anapokataa au kuchelewa kukupa unachoomba ni kwa sababu ya kuimarisha imani yako. Kubali majibu ya Mungu kwa imani na shukrani. Mungu anajua kile anachofanya. Zungumza na Mungu. Anakusikiliza. Omba!

**"Shukuruni kwa kila jambo, kwa maana haya ndio mapenzi ya Mungu kwa ajili yenu katika Kristo Yesu." 1 Wathesalonike 5:18**

---

*Je, Ni Jinsi Gani Napaswa Kuomba?* © 2026 imeandikwa na John D. Morris III na kuchapishwa na Acts One Eight. Unaweza kuichapisha, kuinakili, kuichapisha mitandaoni, kuituma kupita barua pepe, au kuituma kama ujumbe bila kubadilisha maudhui yake huku ukijumuisha kauli hii kikamilifu. Unaweza kujumuisha jina la huduma au kanisa lako au nembo yako kwenye sehemu ya juu ya ukurasa wa kwanza na uweke taarifa zako za mawasiliano juu ya mstari mzito ulio karibu na sehemu ya chini ya ukurasa wa pili. Mafundisho ya Sacrifice316 yanatokana na Biblia pekee. Ipo ili kusaidia watu kuomba na kukua katika uhusiano wao na Mungu. Unaweza kutuma barua pepe kwa Acts One Eight (katika lugha ya Kiingereza ikiwezekana) ukitumia anwani ifuatayo: *Hello@Mail316.org*. Huduma za utafsiri zimetolewa na www.ChristianLingua.com. *Je, Ni Jinsi Gani Napaswa Kuomba?* inapatikana katika lugha 48 bila malipo kwenye *www.Prayer316.org*. Nukuu za Maandiko katika tafsiri hii zimetolewa kutoka kwenye Biblia ya Neno.